

HOTUBA YA MWENYEKITI WA BODI CHUO CHA ARDHI MOROGORO PROFESA SYLIVESTER MPANDUJI

ILİYOTOLEWA KWENYE MAHAFALI YA THELATHINI NA TANO YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO TAREHE 24/03/2017

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa niaba ya Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro, Uongozi wa Chuo, Wanajumuiya na kwa niaba yangu binafsi, Napenda kuchukua nafasi hii, kuwakaribisha wote kwenye Mahafali ya Thelathini na tano ya Chuo cha Ardhi Morogoro. **Karibuni.**

Aidha Napenda kuwashukuru wageni wote waalikwa kwa kukubali kujumuika nasi. Shukrani za pekee nazitoa kwako Dkt. Moses Kusiluka naibu Katibu Mkuu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa mgeni rasmi katika mahafali haya. **Asante sana.**

Vile vile nawashukuru wazazi, walezi, ndugu, jamaa, marafiki na wahitimu wote kwa kulipa ada, kuwaleta vijana wao kusoma katika chuo chetu na kubwa zaidi kwa kushiriki katika sherehe hi muhimu ya kutunukia vyeti wahitimu wetu wa kozi za Jiomatikia. **Asanteni sana.**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana uongozi wa Chuo, wakufunzi, wafanyakazi na wanafunzi wa Chuo wote kwa kudumisha amani, utulivu na ushirikiano, na kubwa zaidi kwa kutoa ushauri na huduma za kitaalamu kwa wananchi na taasisi mbalimbali nchini kote. **Hongereni sana.**

Pia, Napenda nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati wahitimu wote **171** walioweza kumaliza masomo yao katika fani ya Upimaji Ardhi ambao leo hii watatunukiwa vyeti vyao yaani wahitimu wa Cheti cha awali ni **41**, Astashahada ni **70** na stashahada ni **60**. **Wote hongereni sana.**

Nawatakia kila la heri katika ujenzi wa Taifa letu. Aidha nawashukuru sana wananchi na wadau wote wa Ardhi kwa kuendelea kutumia huduma na ushauri unaotolewa na Chuo hiki katika Nyanja za Upimaji Ardhi na uandaaji ramani za msingi kwa ajili ya makazi na matumizi mengineyo. **Asanteni sana.**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Majukumu ya Bodi ya Chuo cha Ardhi ni kusimamia, kushauri, kubuni mipango na kuhamasisha maendeleo ya Chuo. Majukumu mengine ya Bodi ya Chuo ni kuhakikisha wafanyakazi wanafanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia dira, shabaha ya Chuo na sera mbalimbali za Taifa letu. Kwa uchache sera hizo ni pamoja na;-

- Sera ya Taifa ya Ardhi,
- Sera ya Mazingira,
- Sera ya Sayansi na Technolojia,
- Sera ya Elimu na Mafunzo,
- Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi,
- Sera ya Madini ya Taifa,
- Sera ya Serikali za Mitaa na,
- Sera ya Taifa ya Barabara

Kwa nyakati tofauti Chuo kimeweza kutekeleza na kutafsiri kwa vitendo sera hizi, mathalani, Chuo kimeweza kubadili mfumo wa mafunzo kukidhi matakwa ya soko na yale ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Vile vile kutoa huduma ya kupima viwanja katika Halmashauri mbalimbali kwa mfano: Morogoro – Bigwa, Kingolwira, Sangasanga na Kihonda. Pamoja na mikoa mbalimbali kama vile Kagera, Singida, Geita Tanga na Kigoma.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Mwelekeo uliopo wa kupima kila kipande cha Ardhi ili kuwezesha kukuza uchumi wa viwanda, Chuo kinahitaji kuboresha miundo mbinu na raslimali watu ili kuendana na kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi yetu.

Chuo kwa kuona hilo kimebuni mikakati ya muda mfupi na muda ambayo ni:

- Kuongeza kasi ya udahili wa Wanafunzi,
- Kuendeleza eneo la hekta tisa (9) lililoko Mlimakola katika Manispaa ya Morogoro kwa lengo la kupunguza matatizo ya miundombinu,
- Kusomesha Wakufunzi na Wafanyakazi wengine katika ngazi ya shahada za uzamili na uzamivu kwa lengo la kujenga uwezo wa Kitaaluma.
- Kukamilisha uandaaji wa mitaala ya Mipango Miji kwa lengo la kuharakisha upangaji Miji ambayo inakua kwa kasi.
- Kutoa Mafunzo ya muda mfupi kuhusu utatuzi wa migogoro ya Ardhi, na matumizi ya vifaa vya kisasa vya Upimaji Ardhi.
- Kuboresha Muundo wa Utumishi kwa wafanyakazi wa chuo.
- Kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano 2017-2022.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Ni matumaini yangu na Bodi ya Chuo kuwa utakuwa bega kwa bega nasi katika kusaidia utekelezaji wa mikakati niliyoielezea hapo juu hususani kwa kupata wafadhili wa ndani na wa nje ya nchi. Aidha nakuomba wewe binafsi uwe balozi wetu katika upanuzi wa Chuo na kutafuta wafadhili kwa ajili ya masomo ya juu.

Baada ya kusema haya, Napenda nihitimishe hotuba yangu kwa kukushukuru wewe binafsi na wageni wote waalikwa kwa kukubali mwaliko wetu. Nawashukuru Wajumbe wa Bodi kwa ushirikiano wao mzuri na Wanajumuiya ya Chuo cha Ardhi Morogoro walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha Mahafali haya. Mwisho nakuomba kwa heshima na taadhima kubwa utumie fursa hii kuongea na hadhara iliyopo mbele yako na baadaye uwatunuku vyeti wahitimu **171** wa kozi za Upimaji Ardhi na Ramani wa Chuo cha Ardhi Morogoro.

Asanteni kwa kunisikiliza na Karibuni sana.